ANSAF

Agricultural Non State Actors Forum

# TUKIO LA KUJIFUNZA LA 14 LA KILA MWAKA

## BAADA YA MKUTANO WA JUKWAA LA MIFUMO YA CHAKULA BARANI AFRIKA (AFSF) 2023: KUTUMIA FURSA ZINAZOJITOKEZA.




**22 - 23 NOVEMBA 2023**
**DODOMA**

AGRA Growing Africa's Agriculture
Funded by the European Union
fcs FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY Facilitating Partnerships for Development
actionaid
Beyond Farming Collective
gain Global Alliance for Improved Nutrition
Vi Agroforestry
MEDA
NORGES VEL
VOAG

# 1.0 Utangulizi

## 1.1 Muktadha

Jukwaa la wadau wa kilimo (ANSAF)[1] ni shirika lisilo la kiserikali linaloundwa na mashirika mwamvuli ya wakulima, makampuni binafsi na mashirika kiraia ya kitaifa na kimataifa yanayofanya kazi kwenye sekta ya Kilimo nchini Tanzania. Dhumuni la ANSAF ni kubadili maisha ya wazalishaji wadogo kupitia uwekezaji wenye tija na wa kimkakati unaochagizwa na sera na mazingira rafiki ya kibiashara, utawala bora na usimamizi mzuri wa shughuli za kilimo.

Matukio ya kujifunza ya kila mwaka ya ANSAF maarufu kama "Annual Learning Events (ALE)" ni miongoni mwa majukwaa muhimu yanayotumiwa kupata ushahidi wa kushawishi mabadiliko katika sera na utekelezaji wake. ANSAF, kwa kushirikiana na wanachama na washirika wake iliandaa ALE yake ya 14 iliyofanyika tarehe 22 na 23 Novemba 2023 jijini Dodoma, ikiwa na kauli mbiu: ***"Baada ya Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AFSF) 2023: Kutumia Fursa Zinazojitokeza."***

Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AFSF) ambalo awali lilijulikana kama Jukwaa la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRF), lilifanya mkutano wake wa 13 wa kila mwaka kuanzia tarehe 5 hadi 8 Septemba 2023, jijini Dar es Salaam, Tanzania. Mkutano huo ulijikita kwenye maendeleo ya mifumo ya chakula ya Afrika na uhuru wa chakula, vijana na wanawake wakiwa kiini cha maendeleo hayo. Mkutano huu ulihusisha wadau mbalimbali wapatao 5,400 kutoka taasisi za kifedha, wadau wa maendeleo, wafadhili, serikali, watafiti, wawekezaji, na wajasiriamali kutoka Afrika, ukiipa Tanzania fursa ambayo ilivutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (Foreign Direct Investment) katika sekta ya kilimo.

Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AFSF) ulibainisha mafanikio ya Afrika kisiasa, kisera na kifedha katika kujenga mifumo ya chakula yenye tija, lishe, jumuishi, stahimilivu, na endelevu. Mkutano huo ulisisitiza juu ya kutanua wigo wa suluhu muhimu zilizopo ili kuchochea mageuzi ya mifumo ya chakula, kuongeza juhudi za kukuza uzalishaji kupitia njia za kilimo endelevu kwa mujibu wa tamko la Nairobi juu ya mabadiliko ya tabianchi (Nairobi Declaration on Climate Change), kufanya upya nia ya kisiasa ya kuimarisha nafasi za wanawake na vijana katika kujenga mifumo ya chakula inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, kufafanua na kupitisha ahadi za kisiasa zinazoathiri maendeleo na uwekezaji katika uzalishaji wa chakula, masoko, na biashara, uhamasishaji wa kifedha ili kuwezesha biashara za kilimo zinazoongozwa na wanawake na vijana, na kutathimini mafanikio yaliyopatikana katika kubadilisha na kufanya mageuzi ya mifumo ya chakula.

Dhamira ya serikali ya kuongeza jitihada na hamasa ya kuboresha sekta ya kilimo, pamoja na mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AFSF/AGRF) yenye hadhi kubwa, inatoa fursa muhimu kwa Tanzania kupiga hatua kubwa katika kufikia malengo yake ya Ajenda 10/30. Ili nchi itumie ipasavyo fursa zilizotokana na AFSF/AGRF na kuboresha mfumo wake wa chakula, ni muhimu kufanya jitihada za pamoja za kuongeza uelewa miongoni mwa wadau, ikiwemo wazalishaji wadogo, vijana, wanawake, na sekta binafsi. Pia, ni muhimu kushughulikia mapungufu yoyote ambayo yanaweza kuzuia wadau kutumia fursa zinazotokana na tukio hilo kubwa. Hivyo, ANSAF ilitumia tukio lake la 14 la kujifunza ili kutoa nafasi kwa wanachama wake, wazalishaji, sekta ya umma, makampuni binafsi, watafiti, washirika wa maendeleo, wafadhili, na wadau wengine muhimu kutafakari juu ya AFSF/AGRF.

---

[1] www.ansaf.or.tz

## 1.2 Malengo ya Tukio la Kujifunza la Mwaka 2023 (ALE 2023)

ALE ilikusudia kuchochea mijadala na mashauri yaliyolenga kuboresha sera na utekelezaji wake kwenye mfumo wa chakula. Hususani,

- ALE ilichambua fursa zitokanazo na AFSF/AGRF, kwa msisitizo maalum katika kuangalia mikakati ya Tanzania kuzitumia.
- ALE iliwezesha kubadilishana maarifa na kujengeana uwezo miongoni mwa washiriki. Ilihimiza ubadilishanaji wa mawazo, uzoefu na mbinu bora, ili kuwezesha wadau kujifunza wao kwa wao na kupata taarifa kuhusu maendeleo na ubunifu mpya katika kilimo.
- Mambo muhimu yatokanayo kwa ALE yataongoza mipango ya utetezi inayolenga kushawishi sera na utekelezaji wake katika sekta ya kilimo. Kwa kutoa mapendekezo yenye ushahidi na maarifa yanayotekelezeka, ALE inachangia katika uundaji wa sera na mikakati inayozingatia mahitaji yaliyopo.

Ili kufanikisha majadiliano ya kina pamoja na kupata mapendekezo na hatua za kisera, mada ya ALE iligawanywa katika mada ndogo tatu zifuatazo:

1. **Fursa zinazojitokeza** ili kutathmini na kuongeza uelewa wa fursa zilizozalishwa na mkutano wa AFSF/AGRF.
2. **Ushirikishwaji wa wanawake na vijana** ili kuangalia fursa za kipekee ambazo AFSF/AGRF imeleta kwa wanawake na vijana wa Tanzania ndani ya mfumo wa chakula.
3. **Vipande vinavyokosekana** kujadili maeneo ya kisera na kitaasisi ambayo yanahitaji kuzingatiwa ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na fursa zinazojitokeza.



*Mwanachama wa ANSAF - Bi. Tumpale Mahegema kutoka UWAKORU akichangia jambo.*

ALE inaangalia maeneo ya kisera na kitaasisi yanayohitaji maboresho ili kuwezesha nchi kufikia malengo yake katika mageuzi ya mfumo wa chakula. Kwa kutathimini maeneo haya na kutengeneza mikakati ya maboresho, tukio hili lililenga kufungua njia kwa utekelezaji na sera za kilimo zenye tija na ufanisi zaidi, na kuchangia katika usalama wa chakula, maendeleo ya kiuchumi, na ustawi wa jamii za Kitanzania.

## 2.0 Maelezo ya tukio

Ikiwa uwanja muhimu wa majadiliano shirikishi ya kisera ya kuleta mabadiliko chanya na maendeleo katika sekta ya kilimo nchini Tanzania, ALE ilikutanisha washiriki 170 (wanawake 57 na wanaume 113) kutoka taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wanachama na wasio wanachama wa ANSAF, vyama vya wakulima na wafanyabiashara wa kilimo, Wizara zinazofanya kazi kwenye sekta ya kilimo, taasisi za serikali, makampuni binafsi, taasisi za vijana, mashirika ya kiraia, taasisi za elimu na utafiti, washirika wa maendeleo, na vyombo vya habari. Orodha ya washiriki inapatikana hapa. Tukio hili pia lilihusisha takribani washiriki 250 kwa njia ya mtandao kwa kurushwa mubashara kupitia chaneli ya ANSAF ya YouTube and Voice of Agriculture.

Tukio hili lilihusisha vipindi vya majadiliano ya jumla vilivyofanyika baada ya mawasilisho kwa kila mada ndogo, vilivyolenga njia za vitendo za kushughulikia changamoto za msingi. Kulikuwa na vipindi viwili vya majadiliano ya jumla siku ya kwanza na kipindi kimoja kwa siku ya pili. Katika vipindi hivi, kulikuwa na mawasilisho, yakifuatiwa na majadiliano ya jopo yaliyowakutanisha wataalam mbalimbali katika mada ndogo husika. Tukio pia lilihusisha maonyesho na vyombo vya habari.





ALE ililenga kusisimua ushiriki katika majadiliano kati ya washiriki, kubadilishana uzoefu na kujengana kutokana uzoefu wa kila mmoja. Mwishoni mwa tukio, washiriki walishirikiana katika kutambua mambo muhimu yatakayosaidia katika shughuli za utetezi zilizolenga kuboresha sera na utekelezaji kulingana na mada kama ilivyoanishwa sehemu ya nne ya ripoti hii.

ALE 2023 iliratibiwa na ANSAF na washirika wake wa kimkakati ambao wanafanya kazi moja kwa moja kwenye mfumo wa chakula nchini Tanzania. Ushirikiano mzuri na ufadhili wa kifedha kutoka kwa taasisi na watu binafsi ndiyo sababu kuu ya mafanikio ya tukio hili. Hii ilijenga umiliki wa pamoja wa tukio hilo kwa ajili ya kujifunza, kushirikishana maarifa, na kuunda mtandao na wadau wengine. ALE 2023 ilidhaminiwa na AGRA, MEDA Tanzania, GAIN Tanzania, Action Aid Tanzania, mradi wa Beyond Farming Collective (BFC) chini ya Apex Agribusiness Academy, Voice of Agriculture (VOAG) na Norges Vel Tanzania.

## 2.1 Ukaribisho



Mwezeshaji wa tukio Bw. Obey Nkya alifanya utambulisho wa jumla na kutoa shukrani kwa washiriki wote. Kisha alimkaribisha Bw. Honest Mseri - Mkurugenzi Mtendaji wa Muda wa ANSAF, kwa ajili ya ukaribisho. Bw. Mseri aliwakaribisha washiriki na kufafanua malengo ya ALE ambayo yameelezewa katika sehemu 1.2. Aliangaza ALE kama jukwaa muhimu kwa kukuza ushirikiano, kuleta mabadiliko chanya, na kuunda upya mustakabali wa kilimo nchini Tanzania. Wasilisho lake linapatikana hapa.



Mwezeshaji alimkaribisha Bw. Edmond Ringo – Mwenyekiti wa Bodi ya ANSAF ambaye alitoa shukrani zake kwa mgeni rasmi, wanachama wa ANSAF, na washiriki wengine kwa uwepo wao. Alisisitiza umuhimu wa kutumia fursa zilizopo kwenye mfumo wa chakula ili kuhakikisha maendeleo ya sekta ya kilimo na usalama wa chakula hususani kupitia sera bora na wadau kushiriki kikamilifu. Hotuba yake inapatikana hapa.



Kisha mwezeshaji aliwakaribisha wadhamini wawili wa tukio kwa maneno ya ukaribisho. Bi. Lilian Mosha kutoka Mennonite Economic Development Associates (MEDA) Tanzania alitoa maelezo mafupi kuhusu MEDA kwa washiriki akielezea majukumu an kazi yake katika sekta ya kilimo. Alihimiza juu ya umuhimu wa juhudi za pamoja na kujifunza kati ya wadau wa kilimo.



Bw. Saddam Alfani kutoka Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN) Tanzania alielezea majukumu na kazi za GAIN katika kutokomeza utapiamlo. Alipongeza ushiriki wa vijana kwenye ALE na kuwahimiza washiriki vijana kutumia vizuri jukwaa la ALE kwa kwa ajili ya kuunda mtandao na kujifunza kutoka kwa wazee na wataalamu.



Baada ya ukaribisho, mwezeshaji alimkaribisha Bw. Nyasebwa Chimagu - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao, Wizara ya Kilimo amkaribishe Mgeni Rasmi. Bw. Chimagu aliipongeza serikali kwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa AGRF/AFSF ambao ulionyesha uwezo wa Tanzania wa kuvuka matarajio na kusisitiza juu ya kauli mbiu ya mkutano huo - "Rejesha, Unda upya, na Chukua Hatua: Suluhu za Afrika kwa Mabadiliko ya Mifumo ya Chakula".

Aliangazia dhamira ya serikali katika kuleta mabadiliko ya kisekta, ikijumuisha juhudi kadhaa ikiwemo uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji na program ya jenga kesho iliyo bora kwa ajili ya vijana na wanawake (BBT). Pia alisisitiza umuhimu wa kukuza uaminifu, uwazi, na ushirikiano kwenye minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo, na kuwashirikisha vijana ili kutumia fursa za biashara, kuhakikisha mifumo endelevu ya chakula, na kukuza uaminifu katika jitihada za sekta binafsi. Hotuba yake inapatikana hapa.

## 2.2 Ufunguzi

Mgeni Rasmi Dkt. Daniel Elius Mushi - Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alifungua rasmi tukio hili. Dkt. Mushi aliipongeza ANSAF kwa kutumia Tukio lake la Kujifunza la kila Mwaka (ALE) kutafakari juu ya Mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AFSF/AGRF) wa mwaka 2023. Alitoa pongezi zake kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya kuhakikisha maendeleo ya sekta ya kilimo kupitia jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa mwenyeji wa mkutano wa AFSF/AGRF, kuongeza rasilimali za umma kwenye sekta ya kilimo na kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji.

Dr. Mushi alisisitiza haja ya dharura ya kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo, kuboresha ubora, upatikanaji na ugavi wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, kupunguza utegemezi mkubwa wa pembejeo za kilimo zinazoagizwa kutoka nje, mafuta ya kula na ngano, na kuongeza thamani ili kuongeza ajira na mapato kupitia jitihada za pamoja katika biashara na teknolojia bora. Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano, uwekezaji wa kimkakati, na sera jumuishi katika kuchochea maendeleo sekta ya kilimo ya Tanzania. Aliwaasa washiriki kutumia jukwaa la ALE ipasavyo kwa kutoa maoni na mapendekezo kwa serikali ili kuweka mazingira bora ya uwekezaji wa ndani na wa kigeni, na kuwezesha mabadiliko ya mfumo wa chakula.




***Dkt. Daniel Elius Mushi - Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi akihutubia.***

## 2.3 Neno la shukrani

Kwa niaba ya wanachama wa ANSAF, Bw. Hassan Rangi kutoka shirika la Mission for Improvement and Boosting Organizational Services to the Community (MIBOS), alitoa shukrani kwa Mgeni Rasmi Dkt Daniel Elius Mushi – Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kufungua ALE.

# 3.0 Masuala Muhimu, Mapendekezo na Majadiliano

## 3.1 Wasilisho kuu: “Mageuzi ya Mfumo wa Chakula: Muktadha wa Tanzania”.

Dkt. Honest Kessy - Mkurugenzi wa Usalama wa Chakula Kitaifa na Mratibu wa Mifumo ya Chakula nchini Tanzania, alitoa muhtasari wa kina juu ya mageuzi ya mifumo ya chakula kwa muktadha wa Tanzania. Alisisitiza lengo kuu la nchi kufikia mfumo wa chakula wenye tija, usawa, na stahimilivu ifikapo 2030 kupitia njia zilizoainishwa ambazo zinahusisha uimarishaji wa uzalishaji, kushirikisha sekta ya kibinafsi, matumizi ya dijitali, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Alipongeza mafanikio ya nchi hususani kuongezeka kwa nia kisiasa na utengwaji wa wa rasilimali za umma, na kusisitiza juu ya juhudi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na mifumo ya uratibu na ushirikishwaji wa jamii.



Dkt. Kessy alisisitiza juu ya ushirikishwaji wa watendaji wasio wa kiserikali kama vile taasisi za kibiashara, asasi za kiraia na jamii na kuangazia fursa za ufadhili kutoka vyanzo mbalimbali vikiwemo vya ndani pamoja na mashirika ya kimataifa kama IFAD na Benki ya Dunia, hususani kwa sasa ambapo hakuna utaratibu wa ufadhili wa kikapu (Basket Funding) kwa ajili ya mageuzi ya mfumo wa chakula.

Alitoa wito wa kuhusisha jamii za wenyeji moja kwa moja ili kuchochea mageuzi ya mifumo ya chakula na matumizi mazuri ya rasilimali kupitia uratibu mzuri. Wasilisho lake linapatikana hapa.

## 3.2 Mawasilisho na Majadiliano

### 3.2.1 Mada ndogo 1: Tathimini: Fursa zinazojitokeza kwenye Mkutano wa AFSF/AGRF.



Kipengele hiki kiliwezeshwa na Dkt. Sizya Lugeye kukiwa na mawasilisho juu ya fursa zilizojitokeza kwenye AFSF/AGRF. Wasilisho la kwanza lilifanywa na Bi. Adella Ng’atingwa – Kaimu Naibu Mkurugenzi Idara ya Sera na Mipango, Wizara ya Kilimo, na wasilisho la pili Bi. Upendo Hamidu – Afisa Mwandamizi wa Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kulifuatia majadiliano ya jopo, ambayo yaliwahusisha Bw. Moses Kabogo kutoka Lutheran World Relief, Bw. Jackson Mahenge kutoka DALBERG, na Bw. Mussa Khamis Khamis kutoka Zanzibar Organic Farming Association (OFA/UHAI), kisha majadiliano ya pamoja.

Yafuatayo ni mafanikio na fursa zilizotokana na mkutano wa AFSF/ AGRF 2023 kama ilivyobainishwa katika kipengele hiki:

| Sekta Ndogo ya Mazao | Sekta Ndogo ya Mifugo na Uvuvi |
|---|---|
| 1. Uzinduzi wa programu ya Mfumo Himilivu wa Chakula (Tanzania Food System Resilient Programme) 2023/2024 - 2027/2028 wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 300 kutoka Benki ya Dunia. | 1. Ushiriki mkubwa wa wadau wa Mifugo na Uvuvi (takriban washiriki 600) katika mkutano wa AFSF/ AGRF. |
| 2. Ahadi za uwekezaji wa zaidi ya dola za kimarekani milioni 600 kwa ajili ya mradi wa BBT kwa wanawake na vijana kutoka mashirika mbalimbali ikiwemo CRDB, AfDB, AGRA, IFAD, AATI, USAID, na Benki ya Dunia. | 2. Ahadi za Dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Benki ya CRDB kusaidia vijana katika sekta ya mifugo na uvuvi. |
| 3. Wizara ya Kilimo ilisaini makubaliano (MoU) kampuni ya AGRICOM kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kilimo cha makinikia. | 3. Masoko mapya na fursa za uwekezaji kwa watendaji katika sekta ya mifugo na uvuvi walioshiriki katika maonyesho (24) na vyumba vya biashara (12). |
| 4. Wizara ya Kilimo ilisaini makubaliano (MoU) na Benki ya CRDB kwa ajili ya kuanzisha bima ya mkulima katika mnyororo wa thamani wa kilimo. | |
| 5. Wizara ya Kilimo ilisaini makubaliano (MoU) na Norway kwa ajili ya msaada wa utafiti na maendeleo katika kilimo. | 4. Kufikiwa makubaliano na washirika 22 wa maendeleo katika maeneo ya ushirikiano kwa maendeleo ya mifugo na uvuvi |

## Kipengele hiki kilianisha mambo yafuatayo:

| | |
|---|---|
| **Ushiriki wa Vijana:** | • Fursa ziko katika kutoa usaidizi, kama vile mafunzo, upatikanaji wa teknolojia, na kuunda njia kwa vijana kushiriki katika michakato ya maamuzi katika sekta mbalimbali za kilimo. |
| **Fursa za Masoko:** | • Ukaribu na nchi jirani kama vile Congo DRC, Somalia, Sudan na Kenya unatoa fursa za masoko kwa bidhaa za kilimo za Tanzania.<br>• Kupunguza gharama za uagizaji wa chakula kutoka nje, ambao kwa sasa ni zaidi ya dola bilioni 55 barani Afrika, ni njia inayowezekana kuangaliwa katika kukuza uchumi. |
| **Ubora na upatikanaji wa uhakika:** | • Kudumisha ubora na upatikanaji wa uhakika wa bidhaa za kilimo zinayosafirishwa nje imebainishwa kuwa changamoto. Fursa ziko katika kuboresha ubora na upatikanaji wa bidhaa za kilimo, kufikia viwango vya kimataifa, na kuhakikisha upatikanaji wa kutosha kwa masoko ya nje. |
| **Kutumia rasilimali zilizopo:** | • Tanzania ina rasilimali asili nyingi ikiwemo gesi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea ya ndani na hivyo kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi. Kuchunguza na kutumia rasilimali hizi kwa ufanisi kunaweza kuchangia mabadiliko ya sekta ya kilimo. |

| | |
|---|---|
| **Kilimo mseto:** | • Kufanya kilimo mseto, msisitizo ukiwekwa kwenye fursa zaidi ya mazao ya jadi ya kibiashara na chakula. Hii ni pamoja na kukuza kilimo cha bustani, uvuvi, na ufugaji ili kutengeneza mfumo wa chakula unaostahimili zaidi na tofauti. Kukuza kilimo misiti pia ni jambo la msingi. |
| **Teknolojia na Ubunifu:** | • Matumizi ya teknolojia, ikiwa ni pamoja na Teknolojia ya Habari (IT), inatoa fursa za ufanisi katika mfumo wa chakula.<br>• Kusaidia biashara changa za kilimo (startups), hususani zile zinazozingatia teknolojia kunaweza kuchochea uvumbuzi na kuunda fursa za ajira.<br>• Kuna fursa ambazo hazijatumiwa katika uvuvi, ikiwemo uzalishaji wa malisho ya samaki, kutotolesha vifaranga, na kutatua changamoto kama vile athari za shughuli za kilimo katika ufugaji wa samaki. |
| **Ahadi za kifedha:** | • Kuelewa jinsi ya kupata fedha hasa ruzuku na ahadi kutoka kwa wadau wa maendeleo ya kilimo ikiwa ni pamoja na zile zilizoahidiwa kwenye mkutano wa AFSF/AGRF na kuzitumia kwa miradi yenye matokeo ni muhimu kwa maendeleo ya kilimo. |
| **Kuongeza Thamani:** | • Fursa katika uongezaji thamani ikijumuisha upakiaji na uwekaji chapa za bidhaa zinazotengenezwa Tanzania. Kuongeza thamani kutaongeza ushindani katika soko la kimataifa. |
| **Ushirikiano:** | • Ushirikiano kati ya sekta mbalimbali, ikiwemo taasisi za kiserikali, makampuni binafsi, asasi za kiraia, na taasisi za utafiti, ni muhimu. Ubia unaweza kupelekea mikakati ya jumuishi na utekelezaji bora wa sera kwa maendeleo endelevu ya kilimo. |

### 3.2.2 Ushiriki wa Vijana na Wanawake katika Mnyororo wa Thamani ya Kilimo kwa Mfumo wa Chakula Shirikishi.

Kipengele hiki kiliwezeshwa na Bw. Ikunda Teri kutoka Catholic Relief Services (CRS) na kuhusisha wasilisho (linalopatikana hapa) kutoka kwa Dkt. Imani Kapinga - Mkurugenzi Msaidizi wa Kilimo cha Samaki, Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kilifuatiwa na mjadala wa jopo uliowahusisha Bw. Mkali Mlanzi kutoka MEDA, Bi. Loyce Murusuri kutoka Farm Africa, Bi. Loveness Rugiga kutoka Tanzania Horticulture Association (TAHA), na Bi. Hajra Abdul kutoka kwenye jukwaa la vijana, na kisha kufuatiwa ma majadiliano ya pamoja.

Katika maelezo yake, Dkt. Kapinga alibainisha ardhi, maji, rasilimali kazi, na mahitaji makubwa ya soko ndani ya nchi, Jumuiya ya Umoja wa Afrika Mashariki na SADC kama mojawapo ya fursa za uwekezaji katika sekta ya ufugaji wa samaki. Alionyesha jitihada muhimu za serikali ikiwa ni pamoja na kutoa vitendea kazi kwa maafisa ugani, ukarabati na upanuzi wa vituo vya maendeleo ya ufugaji wa samaki, uanzishwaji mashamba darasa (yanayoendeshwa na vikundi vya vijana na wanawake vilivyopatiwa mitaji ya kuanzia) katika kila wilaya, mikopo ya pembejeo isiyo na riba, programu ya BBT-LIFE, mwongozo wa ufugaji wa samaki kwa lugha rahisi ya Kiswahili (unaopatikana hapa), kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha kwa pembejeo za uvuvi, vibali vya bure kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, uanishwaji wa maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki katika maziwa makuu na kuanzishwa kwa dawati la sekta binafsi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuunganisha wakulima na taasisi za kifedha.

**Kipengele hiki kilianisha fursa zifuatazo kwa ajili ya kuimarisha ushiriki wa wanawake na vijana katika mfumo wa chakula:**

| | |
|---|---|
| Utumiaji mzuri wa fursa za ufadhili na programu zilizopo. | • Program ya kuwezesha vijana na wanawake katika sekta ya kilimo, BBT-YIA na BBT-LIFE.<br>• Mikopo (ECF-IMF Loans) ya pembejeo za ufugaji wa samaki, kilimo cha mwani, na boti za uvuvi isiyo na riba kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.<br>• Fursa za kiteknolojia, ujuzi na mitaji kutoka program na mifuko ya kifedha iliyopo SIDO, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) and VETA.<br>• Mikopo ya 10% ya Halmashauri kwa wanawake, vijan ana with wenye ulemavu, ambayo wa sasa imesitishwa kwa muda, na Waziri mkuu alitoa maelekezo irudishwe kufikia Januari 15, 2024 |
| Uhamasishaji wa vijana na wanawake. | • Kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika na vyama vya kuweka na kukopa vya vijana na wanawake ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za kifedha. Tunaweza kujifunza kutoka kwa mifano iliyopo kama vile ushirika wa wanawake wa MADIRISHA. |
| Mkakati Jumuishi wa Kina wa Ushiriki wa Vijana katika Mkakati wa Mfumo wa Chakula | • Wakati jitihada mbalimbali za serikali, kama vile BBT ipo kwa ajili ya kukuza ushiriki wa vijana katika kilimo, kutakuwa na haja kubwa ya mkakati jumuishi wa kina. Mkakati huu utasaidia nchi kutumia kwa ufanisi fursa katika sekta zote ndogo za kilimo, kuhakikisha uwiano, kuimarisha uratibu, na mwingiliano kisekta katika siku zijazo. |
| Uwepo wa masoko kutokana na uhitaji mkubwa wa bidhaa za kilimo. | • Mahitaji makubwa ya malisho ya samaki ambayo kwa sasa uhitaji unafikia 27,000+ MT, na vifaranga vya samaki ambayo mahitaji ya sasa ni milioni 35. (Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalenga zaidi ya vifaranga milioni 85 ifikapo 2025).<br>• Fursa za uchakataji na kuongeza thamani ikijumuisha usindikaji wa angalau 90% ya MT 5,000 za mwani unaulimwa kwenye mabwawa, vizimba na matangi (Wizara inalenga 50,000 MT za samaki kufikia 2025 kutokana na uzalishaji wa sasa wa 33,525.46 MT). |

### 3.2.3 Mada ndogo 3: Kutengeneza Mazingira Wezeshi kwa Mageuzi ya Mfumo wa Chakula Tanzania.

Kipengele hiki kiwezeshwa na Bi. Judith Valerian kutoka Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Kilianza na wasilisho juu ya ubunifu unaohitajika katika sera na utawala kwa ajili ya mageuzi ya mifumo ya chakula jumuishi na endelevu kutoka kwa Bi. Aneth Kayombo kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO). Wasilisho lake linapatikana hapa.

Kilifuatiwa na majadiliano ya jopi yaliyowahusisha Bi. Linda Temba kutoka Island of Peace (IDP), Bw. Lawrence Kitogo kutoka Environmental Management and Economic Development Organization (EMEDO), Bi. Rose Lyimo kutoka Chama cha Wasindikaji wa Maziwa nchini (TAMPA) na Bw. Geofrey Rwiza kutoka Baraza la Zao la Mchele Tanzania (RCT), na kisha majadiliano ya jumla.

**Wasilisho la Bi. Aneth kutoka FAO liliangazia mambo muhimu yafuatayo:**

- **Uratibu duni:** Uratibu duni kati ya sekta zinazohusiana na kilimo, biashara, afya na mazingira ambao unazuia mbinu za umoja na ujumla.
- **Umiliki wa ardhi:** Sehemu kubwa ya ardhi inamilikiwa na kudhibitiwa na wanaume hasa wazee ambapo inapunguza upatikanaji wa ardhi kwa wanawake na vijana.
- **Mapungufu katika sera ya biashara:** Sera za biashara zinazopekelea mauzo ya bidhaa ghafi kwenda nje nchi kuliko bidhaa zilizoongezewa thamani huzuia uchakataji wa ndani na kufifisha uwekezaji akitoa mfano kwa zao la alizeti na korosho.
- **Vikwazo vya kikanuni:** Vikwazo vya Udhibiti: Urasimu na kanuni ngumu huzuia uwekezaji, biashara na matumizi ya teknolojia za kibunifu, hususani kwa wakulima wadogo na biashara ndogo na za kati.

**Mapendekezo ya kuboresha mazingira wezeshi:**

- **Upatikanaji wa Fedha:** Kuwezesha upatikanaji rahisi wa fedha kwa ajili ya biashara, hasa biashara ndogo na za kati (SMEs). Hii inaweza kuhusisha uundaji wa mipango ya udhamini wa mikopo, kusaidia mbinu mbadala za ufadhili, na elimu ya fedha. Hizi ni pamoja na kurejesha na kuimarisha uendeshaji wa mfuko wa mikopo ya Halmashauri ya 10% ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
- **Usaidizi wa kuanzisha biashara:** Kutengeneza mfumo unaosaidia wajasiriamali na wanaoanzisha biashara. Hii ni pamoja na incubators za biashara, programu za ushauri na fursa za kukuza mitandao ili kusaidia biashara mpya kukabiliana na changamoto.
- **Mboresho ya kikodi:** Utekelezaji wa mipango ya kupunguza ugumu wa taratibu za kodi, kupunguza viwango vya kodi, na kuondoa mizigo isiyo ya lazima. Mfumo wa kodi wa haki unachochea uzingatiaji.
- **Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPPs):** Kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kushughulikia changamoto za pamoja na kuunda maelewano. Ubia huu unaweza kupelekea utoaji wa huduma kwa ufanisi zaidi na maendeleo ya miundombinu.



# 4.0 Mambo ya Kujifunza na Mapendekezo.

## 4.1 Mambo ya Kujifunza.

- **Umuhimu wa uratibu, taarifa na kujifunza:** Kuleta pamoja watendaji mbalimbali kunakuza maafikiano, kujifunza kwa pamoja, na kubadilishana mawazo na uzoefu kati yao kunachangia maboresho endelevu na ufanyaji maamuzi unaozingatia taarifa.
- **Uwezeshaji wa Vijana na Wanawake:** Tukio hili lilisisitiza majukumu muhimu ya vijana na wanawake katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Kutambua na kuwezesha kundi hili ni muhimu kwa ukuaji endelevu na shirikishi.
- **Fursa za masoko:** Kutafuta na kukuza fursa za masoko, ndani na nje ya nchi ni muhimu katika kupunguza uagizaji wa bidhaa za chakula kutoka nje ya nchi, kuhamasisha matumizi ya bidhaa za ndani, na kukuza uchumi wa kilimo.
- **Ubora na Uthabiti:** Kuhakikisha ubora, uthabiti, na wingi wa uzalishaji wa kilimo ni muhimu ili kukidhi mahitaji ya masoko. Hatua za pamoja na pembejeo zilizoboreshwa ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha ubora na wingi wa mazao kwa ujumla.
- **Ubunifu: Innovation:** ALE iliangazia umuhimu wa ubunifu, teknolojia na zana za kisasa katika kuboresha ufanisi katika mfumo wa chakula. Uanzishaji wa vituo vya ufundi mashine na kukuza uanzishwaji wa biashara za teknolojia ya kilimo ni mikakati muhimu.
- **Kilimo kinachozingatia tabianchi:** Kushughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi kupitia mbinu za kilimo kinachozingatia tabianchi ni muhimu. Tukio hili lilisisitiza uhitaji wa kuimarisha ustahimilivu wa mabidiliko ya tabianchi.
- **Kuongeza thamani:** Uzalishaji wa mazao ya kilimo mseto na kuongeza thamani kwa bidhaa zilizopo huchangia katika sekta iliyo imara na yenye ushindani. Mbinu hii pia inaweza kufungua fursa mpya za soko.
- **Ahadi za Serikali:** ALE ilisisitiza umuhimu wa ahadi za serikali katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Utayari wa serikali kuwekeza katika miundombinu, umwagiliaji na utengenezaji wa ajira unaashiria mwelekeo mzuri kwa sekta hiyo.
- **Sera Jumuishi:** ALE iliangazia haja ya sera jumuishi zinazozingatia mnyororo mzima wa thamani, ikijumuisha usafirishaji, miundombinu husika, biashara, na sekta zinazohusiana. Ushirikishaji katika uundaji wa sera huhakikisha kwamba wadau mbalimbali wanazingatiwa.
- **Utetezi wa Sera:** ALE ilisisitiza jukumu muhimu la utetezi wa sera katika kuendeleza sauti ya wadau wa kilimo. Kushirikiana na serikali na kutetea sera bora kunaweza kuleta maendeleo ya sekta hii.

## 4.2 Mapendekezo

1. Licha ya programu zilizopo za BBT katika mazao na mifugo, na mpango ujao wa ufugaji nyuki, mkakati wa kina unahitajika ili kukabiliana na ukosefu wa ajira kwa vijana na kuwashirikisha ipasavyo katika mageuzi ya mifumo ya chakula.
2. Kuongeza ya serikali kwenye sekta ya kilimo ili kufikia utengaji wa 10% ya bajeti yote ifikapo 2030, na kuhakikisha utoaji wa bajeti hiyo kwa wakati na wa kutosha kwa maeneo muhimu ili kufikia ukuaji wa 10% kwa sekta ifikapo 2030.
3. Uwekezaji wa kifedha uambatane na sera na kanuni wezeshi. Hii inajumuisha uundwaji wa sheria ya kilimo cha mkataba, na mapitio ya sheria za umwagiliaji na sheria ya vyama vya ushirika.
4. Kusaidia wazalishaji wadogo kuchangamkia fursa za biashara ndani ya AfCFTA, SADC, EAC, na kwingineko kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara na kuimarisha mashirika ya wakulima, vyama vya ushirika, na biashara ndogo ndogo za kilimo na za kati.

5. Ili kutengeneza mfumo endelevu wa chakula na kushughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi, ni muhimu kukuza ufadhili na mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inayotolewa kwa ruzuku, inayoongozwa na wenyeji, jumuishi, inayozingatia jinsia, na inayozingatia wakulima wadogo.
6. Kusambaza ajenda ya mfumo endelevu wa chakula katika ngazi za Halmashauri na kuimarisha utoaji wa huduma za ugani. Ushahidi kutoka kwenye mfumo wa kidigitali wa M-Kilimo unaonyesha kuwa mfumo wa jadi wa utoaji huduma za ugani haupaswi kupuuzwa. Maafisa ugani wapatiwe vifaa na rasilimali za kutosha, na marekebisho ya majukumu yao kuzingatiwa kikamilifu.
7. Kuimarisha miundombinu ya vijijini, ikiwemo barabara, upatikanaji wa nishati, na uhifadhi wa mazao, ili kupunguza hasara baada ya mavuno na kuimarisha usalama wa chakula. Kuanzisha vifaa muhimu vya kutunza baridi kwenye bandari na viwanja vya ndege. Kuendeleza na kutekeleza mkakati wa kina wa usimamizi baada ya mavuno.
8. Kuimarisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa wazalishaji wadogo.
9. Kuwekeza katika maarifa ya tafiti, ikijumuisha teknolojia asilia, ili kuharakisha mageuzi ya mifumo ya chakula.







## 5.0 Hitimisho na Wito

1. Utayari na uwezo wa kubadilisha mfumo wa chakula upo, ni muhimu kushughulikia vipande vilivyokosekana ili fursa hizi zitumiwe ipasavyo.
2. Kuna haja ya kusambaza fursa zinazotokana na AFSF/AGRF zinahitajika katika njia rahisi kwa watumiaji.
3. Wizara husika kusambaza fursa hizi kwa hadhira pana zaidi, ikiwa ni pamoja na wazalishaji wadogo wadogo wa ndani, wanawake, na vijana.
4. Kuanzisha utaratibu wa ufuatiliaji ni muhimu kwa kutambua fursa hizi na kufikia mageuzi ya mifumo ya chakula ya kimfumo na jumuishi.

### Annex 1: Mambo muhimu na Mapendekezo

| Eneo/ Fursa | Changamoto | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Uzalishaji na tija** | • Kupungua kwa rutuba ya udongo.<br>• Gharama kubwa za uzalishaji.<br>• Gharama kubwa za pembejeo za mifugo k.m. chakula cha kuku.<br>• Bajeti ya serikali kwa sekta ya kilimo kutotosheleza mahitaji. | • Kuboresha huduma za upimaji udongo.<br>• Kuimarisha huduma za ugani na kujenga uwezo kwenye teknolojia mpya zaidi.<br>• Kuongeza utoaji wa elimu na teknolojia kwa wazalishaji.<br>• Kuongeza mgao wa bajeti ya serikali kwa sekta ya kilimo kufikia angalau 10% ya bajeti yote kwa mujibu Makubaliano ya Malabo. |
| **Ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.** | • Ushiriki mdogo wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.<br>• Upatikanaji mdogo wa mtaji na fursa za uwezeshaji. | • Kutumia mikopo iliyosimamishwa ya 10% ya Halmashauri ambayo kwa mujibu wa agizo la Waziri Mkuu itarudishwa Januari 15, 2024.<br>• Kuimarisha vyama vya ushirika na vyama vya kuweka na kukopa vya vijana na wanawake. |
| **Masoko na kuongeza thamani.** | • Ufikiaji mdogo wa masoko.<br>• Ubora wa chini wa bidhaa.<br>• Uwekaji chapa na ufungaji usioridhisha.<br>• Ushiriki na ufahamu mdogo.<br>• Gharama kubwa za uingizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini.<br>• Fursa zilizopo katika sekta ya mifugo kutotumiwa ipasavyo. | • Kuongeza thamani ya mazao na mazao ya mifugo kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.<br>• Kuweka sera rafiki kulinda na kukuza uwekezaji na viwanda vya ndani ili kukuza uongezaji thamani na uundaji wa nafasi za kazi. |
| **Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa maendeleo ya biashara.** | • Upatikanaji mdogo wa taarifa juu ya fursa za Serikali ikiwemo Mfuko wa Pembejeo za kilimo (AGITF) na mikopo ya uvuvi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.<br>• Upatikanaji mdogo wa mkopo kwa wazalishaji na watendaji kwenye minyororo wa thamani ya kilimo. | • Kuunda na kukuza fursa za uwezeshaji kwa biashara ndogo na za kati.<br>• Sekta ya fedha kujifunza na kuelewa sekta ya kilimo.<br>• Kuhakikisha fursa za kupata mtaji zinafikia kiwango cha chini.<br>• Ufadhili wa kikapu kwa ASDP II. |

| Eneo/ Fursa | Changamoto | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Mazingira wezeshi (sera, sheria, na kanuni)** | • Kubadilika badilika kwa sera.<br>• Kuna baadhi ya sera zilizopitwa na wakati na zinazokosekana.<br>• Utekelezaji sera usio na ufanisi, kutokuwa na uratibu wa kutosheleza katika taasisi za umma.<br>• Ushiriki mdogo wa wananchi katika uundaji na utekelezaji wa sera.<br>• Sera kutojulikana vyema katika ngazi za chini. | • Kuunda sera zisizobadilika badilika wala kukinzana.<br>• Kuhakikisha michakato jumuishi katika uundaji na utekelezaji wa sera.<br>• Kukuza uelewa kuhusu sera, mipango na fursa.<br>• Uratibu bora wa kodi zinazotozwa na Halmashauri.<br>• Kuimarisha utekelezaji wa sera na uratibu. |
| **Miundombinu ya vijijini** | • Huduma za usafiri na uhifadhi wa mazao yanayoharibika kwa maeneo ya vijijini kutotosheleza kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara.<br>• Kuharibika kwa miundombinu ya barabara.<br>• Ukosefu wa miundombinu ya kuhifadhi. | • Uboreshaji wa usafiri vijijini na umeme/nishati.<br>• Kuwezesha uwekezaji katika mifumo ya kuhifadhi baridi (cold chain). |
| **Usalama wa chakula na lishe** | • Ulaji mdogo wa baadhi ya aina za vyakula ikiwa ni pamoja na maziwa, samaki, na nyama katika soko la ndani ya nchi.<br>• Kutokuwa na uhakika katika usalama wa chakula katika soko la ndani ya nchi. | • Kuhamasisha kampeni za usalama wa lishe na chakula kwa wazalishaji na watumiaji.<br>• Kuhamasisha matumizi ya ndani ya bidhaa za mifugo.<br>• Kuelimisha wazalishaji juu ya viwango vya ubora wa chakula. |



actionaid
Actions for Democracy and Local Governance
AGA KHAN FOUNDATION
Amsha INSTITUTE
ANGONET
BINGO NETWORK

BOSEDA
brac
Café Africa
CRS CATHOLIC RELIEF SERVICES
CEMDO
COSITA

EKAMA DEVELOPMENT FOUNDATION Empowering Women Protecting Children
FARM AFRICA
femina hip
FUO
HELVETAS Swiss Intercooperation
IDINGO
IECA

KAESO
KMCCS LTD
KickStart
KILIMANJARO KDCJE
KILOMBERO ORGANIZATION FOR COMMUNITY DEVELOPMENT
KIMWAM
KPD
PELUM ASSOCIATION Networking for a greener Africa.

Life Change Rukwa Development Organization
Match Maker Associates
MIBOS
Miico EMPOWERING COMMUNITIES
Maasai Pastoralist Development Organization (MPDO - LARETO)
MVIWATA KAGERA
NADO

NatureRipe Kilimanjaro
OPEN MIND TANZANIA
ORSHI ORGANIZATION FOR RURAL SELF-HELP INITIATIVES
RABIKA POULTRY FARM
RCT Rice Council of Tanzania
rikolto
Rukwa Sustainable Development Organization RUSUDEO
RUDI Rural Urban Development Initiatives

SNV Connecting People's Capacities
SUGECO Sokoine University Graduate Entrepreneurs Cooperative
SWISSAID
swisscontact
Tanzania Coffee Association
Tanzania Graduate Farmers Association
TALIA

TANZANIA GENDER NETWORKING PROGRAMME
*Gender Equality, Equity and Social Justice*
TAGRODE
TAHA TANZANIA HORTICULTURAL ASSOCIATION
TAWLAE CARES
TOAM Tanzania Organic Agriculture Movement
TRIAS
TUSHIRIKI
Uhai

Vi Agroforestry
VSO
wajibika
WEPMO WATER FOR LIFE
World Vision